Editon Consortium Journal of Kiswahili [ISSN: 2663 -9289]

**Issue no:** 01 | **Vol no:** 07 | **July** 2026: 51-61

# Yaliyomo katika Jukwaa la *YouTube* kama Wenzo wa Kufundishia Kiswahili katika Elimu ya Vyuo Vikuu: Ushahidi kutoka Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya

**Article History**
Received: **2026.05.12**
Accepted: **2026.06.15**
Published: **2026.07.20**

**Vitalis Sakiti**(1)
**Gladys Kinara**(2)
**Amukowa Deborah**(3)

[1,2]Kibabii University, Kenya; [3]Maseno University, Kenya.
Main author's email: vitaliswanjala24@gmail.com

**Cite this article in APA**
Sakiti, V., Kinara, G., & Deborah, A. (2026). Yaliyomo katika jukwaa la *YouTube* kama wenzo wa kufundishia Kiswahili katika elimu ya vyuo vikuu: Ushahidi kutoka Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya. *Editon consortium journal of Kiswahili, 7*(1), 51–61. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.729

**Ikisiri**
Makala hii ililenga kuchunguza upatikanaji wa *YouTube* katika ufundishaji wa Kiswahili, kubainisha matumizi yake katika ufundishaji huo, na kuchunguza yaliyomo kwenye *YouTube* kama chombo cha kufundishia Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Utafiti ulitokana na matumizi ya teknolojia za kidijitali zinazobadilisha mbinu za ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vikuu, huku *YouTube* ikitokea kama moja ya majukwaa yanayotumika kwa upana kusambaza maudhui ya kielimu. Utafiti uliongozwa na mkabala mseto wa mbinu sambamba. Data za kiai zilikusanywa kutoka kwa wahadhiri 10 na wanafunzi 87 kwa kutumia hojaji. Aidha, video 44 za *YouTube* zilizotumika kama zana za kufundishia Kiswahili zilifanyiwa uchambuzi wa maudhui. Washiriki waliteuliwa kwa kutumia mbinu za usampulishaji za nasibu na za kimakusudi kulingana na sifa za makundi husika. Data za kiasi zilizopatikana zilichanganuliwa kwa takwimu za maelezo (masafa na asilimia), huku data za ubora na maudhui ya video zikifanyiwa uchambuzi wa dhamira na uchambuzi wa maudhui. Matokeo yalionyesha kuwa *YouTube* inapatikana na kutumika kwa kiwango kikubwa katika ufundishaji wa Kiswahili, na ina maudhui yanayohusiana na matamshi, sarufi, msamiati, fasihi na mawasiliano ambayo huongeza uelewa wa wanafunzi, ushiriki wao na ujifunzaji wa kujitegemea. Makala hii inahitimisha kuwa *YouTube* ni chombo muhimu cha kufundishia Kiswahili ikiwa maudhui yake yatahifadhiwa na kutumika kwa mujibu wa malengo ya ufundishaji. Utafiti unachangia maarifa kuhusu matumizi ya *YouTube* katika ufundishaji wa Kiswahili. Unaonyesha kuwa ubora wa maudhui, ulinganifu wake na mtaala, pamoja na uwezo wa walimu kuyachagua na kuyatumia kwa ufanisi, ndizo nguzo za matumizi yenye tija ya *YouTube* katika elimu ya vyuo vikuu.

**Key words**: Elimu ya vyuo vikuuu, Kiswahili, maudhui ya kidijitali, wenzo wa ufundishaji, *YouTube*.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Lengo kuu la utafiti huu ni kufafanua yaliyomo katika *YouTube* kama wenzo wa kufundishia Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii kwa kuchambua jinsi matumizi ya mtandao wa *YouTube* yanavyohusisha shughuli mbalimbali katika ufundishaji wa Kiswahili. Katika miongo miwili iliyopita, maendeleo ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yameleta mageuzi makubwa katika sekta ya elimu kwa kubadili namna ufundishaji na ujifunzaji unavyotekelezwa katika taasisi za elimu duniani. Kuenea kwa teknolojia za kidijitali kumewezesha walimu na wanafunzi kutumia rasilimali mbalimbali za mtandaoni zinazosaidia kujenga ujifunzaji unaomshirikisha mwanafunzi kikamilifu na unaoendelea hata nje ya mazingira ya darasa (UNESCO, 2020). Miongoni mwa majukwaa yaliyopata matumizi makubwa katika elimu ni *YouTube*, ambalo limekuwa chanzo muhimu cha maudhui ya video yanayoweza kutumiwa kufundishia na kujifunza taaluma mbalimbali, ikiwemo Kiswahili. Katika makala hii, *YouTube* inachukuliwa kuwa jukwaa la kidijitali linalowezesha upatikanaji na usambazaji wa maudhui ya video yanayoweza kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika elimu ya vyuo vikuu (Mayer, 2021; Jailani, 2022).

Katika ufundishaji wa lugha, matumizi ya *YouTube* yameendelea kupewa umuhimu kutokana na uwezo wake wa kuwasilisha maudhui kupitia video zinazounganisha sauti, picha, maandishi na vielelezo vinavyorahisisha ujifunzaji. Tafiti mbalimbali zimeonyesha kuwa video za kielimu huongeza ushiriki wa wanafunzi, huimarisha uelewa wa dhana zinazofundishwa, na huwapa wanafunzi fursa ya kujifunza kwa kasi yao wenyewe (Mayer, 2021). Aidha, Jailani (2022) wanabainisha kuwa matumizi ya *YouTube* katika ufundishaji wa lugha huchangia ukuzaji wa stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa kuwa wanafunzi hujifunza lugha katika miktadha halisi ya mawasiliano. Vivyo hivyo, Ratna Rintaningrum (2024) anaeleza kuwa majukwaa ya kidijitali yanayowezesha matumizi ya video huchochea ujifunzaji shirikishi na ujifunzaji huru, hali inayoongeza motisha ya wanafunzi na kuimarisha matokeo ya ujifunzaji wa lugha.

Licha ya kukubalika kwa *YouTube* kama wenzo wa kufundishia lugha, maandishi mengi yaliyopo yamejikita katika matumizi yake katika ufundishaji wa Kiingereza na lugha nyingine za kigeni, huku yakitoa nafasi ndogo kwa Kiswahili, hususan katika elimu ya vyuo vikuu barani Afrika. Aidha, tafiti nyingi zimejikita katika kuchunguza athari za *YouTube* kwa matokeo ya ujifunzaji au mitazamo ya walimu na wanafunzi, badala ya kuchanganua yaliyomo katika video zinazotumika kufundishia lugha. Hivyo, bado kuna upungufu wa ushahidi kuhusu aina za maudhui ya Kiswahili yanayopatikana katika *YouTube* na namna yanavyoweza kutumiwa kufanikisha ufundishaji katika vyuo vikuu nchini Kenya.

Ingawa tafiti zilizotangulia zimeonyesha kuwa *YouTube* ni jukwaa lenye uwezo wa kuimarisha ujifunzaji wa lugha kwa kuongeza ushiriki wa wanafunzi, motisha na ujifunzaji wa kujitegemea, bado kuna mapungufu kadhaa katika fasihi iliyopo. Tafiti nyingi zimejikita katika lugha za kigeni, hususan Kiingereza, na zimechunguza matumizi ya *YouTube* kama teknolojia ya ufundishaji kwa ujumla. Kwa kiasi kikubwa, tafiti hizo hazijachambua aina za maudhui ya Kiswahili yanayopatikana katika *YouTube*, ubora wake, wala namna yanavyoweza kuendana na malengo ya ufundishaji katika elimu ya vyuo vikuu. Zaidi ya hayo, ushahidi kuhusu matumizi ya maudhui hayo katika muktadha wa vyuo vikuu nchini Kenya bado ni mdogo. Pengo hili linaonyesha umuhimu wa kufanya utafiti unaolenga kuchanganua yaliyomo katika *YouTube* kama wenzo wa kufundishia Kiswahili.

Tofauti na tafiti zilizotangulia ambazo zimejikita katika matumizi ya *YouTube* kwa ujumla, makala haya yanachanganua moja kwa moja maudhui ya video za *YouTube* zinazotumika kufundishia Kiswahili katika elimu ya vyuo vikuu na kuyahusisha na maoni ya wanafunzi na wahadhiri. Kutokana na pengo hilo, makala haya yanachunguza yaliyomo katika jukwaa la *YouTube* kama wenzo wa kufundishia Kiswahili kwa kutumia ushahidi kutoka Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya. Lengo kuu ni kubainisha aina za maudhui ya Kiswahili yanayopatikana katika *Yo*uTube, kutathmini mchango wake katika kuimarisha ufundishaji, na kujadili namna yanavyoweza kutumiwa kwa kuzingatia malengo ya kozi na mahitaji ya wanafunzi.

Kwa kufanya hivyo, makala haya yanatoa mchango katika kuongeza maarifa kuhusu matumizi ya maudhui ya kidijitali katika ufundishaji wa Kiswahili, pamoja na kutoa mwongozo kwa wahadhiri, watunga mitaala na taasisi za elimu ya vyuo vikuu kuhusu uteuzi na matumizi ya maudhui ya *YouTube* katika kufanikisha ujifunzaji. Makala haya yamepangwa katika sehemu

tano: utangulizi, mapitio ya maandishi, mbinu za utafiti, matokeo na majadiliano, na hitimisho.

## MAPITIO YA MAANDISHI

### *YouTube* kama Wenzo wa Kufundishia Lugha

Maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yamepanua matumizi ya majukwaa ya kidijitali katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. YouTube imeibuka kama wenzo muhimu miongoni mwa majukwaa hayo kutokana na uwezo wake wa kuwasilisha maudhui kwa kutumia video zinazounganisha sauti, picha, maandishi na vielelezo vinavyorahisisha uelewa wa wanafunzi (Almurashi, 2016). Kwa mujibu wa Mayer (2021), ujifunzaji unaotumia vielelezo vya kuona na kusikia huongeza uelewa wa dhana changamano kwa kuwa wanafunzi hupokea taarifa kupitia njia zaidi ya moja. Mtazamo huu unaifanya *YouTube* kuwa jukwaa linaloweza kuimarisha ujifunzaji unaomshirikisha mwanafunzi kikamilifu.

Tafiti mbalimbali zimeonyesha kuwa matumizi ya *YouTube* huongeza ushiriki wa wanafunzi, motisha ya kujifunza na uwezo wa kujifunza kwa kujitegemea. Alawiyah na Santosa (2022) walibaini kuwa wanafunzi waliotumia *YouTube* walionesha mtazamo chanya kuhusu ujifunzaji wa lugha na waliripoti kuongezeka kwa uelewa wa msamiati na stadi za mawasiliano. Vivyo hivyo, Jailani (2022) wanaeleza kuwa YouTube huchangia kuboresha stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa kuwa wanafunzi hujifunza lugha kupitia matumizi halisi katika mazingira mbalimbali ya mawasiliano. Hata hivyo, tafiti hizi zilijikita zaidi katika ufundishaji wa Kiingereza, hivyo hazikutoa ushahidi wa kutosha kuhusu matumizi ya *YouTube* katika ufundishaji wa Kiswahili.

Kwa upande mwingine, Porto na wenzake (2022) wanasisitiza kuwa teknolojia za kidijitali zinaongeza ujifunzaji shirikishi pale zinapotumiwa sambamba na mbinu za ufundishaji zinazomlenga mwanafunzi. Hoja hii inaafikiana na Berk (2009), ambaye anaeleza kuwa video za kielimu hazipaswi kuchukua nafasi ya mwalimu bali zinapaswa kutumika kama wenzo unaokamilisha mbinu za kawaida za ufundishaji. Kwa hiyo, ufanisi wa *YouTube* hautegemei uwepo wa video pekee, bali unategemea ubora wa maudhui, uteuzi wa video unaofanywa na mwalimu na namna maudhui hayo yanavyounganishwa na malengo ya kozi.

Ingawa maandishi yaliyopo yanathibitisha umuhimu wa *YouTube* katika ufundishaji wa lugha, mengi yamejikita katika kuchunguza matumizi ya jukwaa hilo kwa ujumla badala ya kuchanganua yaliyomo katika video zinazotumika kufundishia lugha. Zaidi ya hayo, tafiti chache zimeangazia Kiswahili katika elimu ya vyuo vikuu nchini Kenya. Hivyo, makala haya yanapanua maarifa yaliyopo kwa kuchunguza aina za maudhui yanayopatikana katika *YouTube* na namna yanavyoweza kutumiwa kama wenzo wa kufundishia Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii.

### Yaliyomo katika Jukwaa la *YouTube* kwa Ufundishaji wa Kiswahili

*YouTube* imeendelea kuwa hazina muhimu ya maudhui ya kielimu yanayotumika katika ufundishaji wa lugha kutokana na uwezo wake wa kuhifadhi na kusambaza video zinazoshughulikia mada mbalimbali za kitaaluma. Tafiti zilizotangulia zimeonyesha kuwa video zinazopatikana katika jukwaa hili huchangia ufundishaji wa vipengele mbalimbali vya lugha, ikiwemo sarufi, msamiati, matamshi, mawasiliano na fasihi (Mayer, 2021; Jailani (2022). Kupitia maudhui hayo, wanafunzi hupata fursa ya kuona matumizi ya lugha katika miktadha halisi, jambo linalorahisisha uelewa wa dhana zinazofundishwa na kuunganisha maarifa ya kinadharia na matumizi ya vitendo.

Pamoja na mchango huo, maandishi mengi yaliyopo yamejikita katika kutathmini athari za *YouTube* katika ujifunzaji wa lugha badala ya kuchunguza yaliyomo katika video zinazotumika kufundishia. Kwa mfano, Alawiyah na Santosa (2022) walijadili mitazamo ya wanafunzi kuhusu matumizi ya *YouTube* katika kujifunza lugha, huku Ratna Rintaningrum (2024) akisisitiza nafasi ya teknolojia katika kujenga ujifunzaji shirikishi. Hata hivyo, tafiti hizo hazikufafanua kwa kina aina za maudhui yaliyokuwa yakitumiwa wala namna maudhui hayo yanavyoweza kuendana na malengo ya ufundishaji wa lugha mahususi kama Kiswahili.

Katika muktadha wa Kiswahili, maelezo kuhusu yaliyomo katika *YouTube* bado ni machache, hususan katika elimu ya vyuo vikuu nchini Kenya. Ingawa kuna ongezeko la video zinazohusu sarufi, fasihi, matamshi, hotuba, ushairi, mijadala ya kitaaluma na matumizi ya lugha katika mazingira halisi, bado hakuna ushahidi wa kutosha unaoonyesha aina za maudhui yanayotawala, ubora wake na namna yanavyoweza kutumiwa kama wenzo wa kufundishia. Upungufu huu unaacha pengo

muhimu katika fasihi kuhusu mchango wa maudhui ya *YouTube* katika ufundishaji wa Kiswahili.

Kwa msingi huo, makala haya yanajenga mchango wake kwa kuchanganua yaliyomo katika video 44 za *YouTube* pamoja na maoni ya wanafunzi 87 na wahadhiri 10 wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Tofauti na tafiti nyingi zilizotangulia ambazo zilijikita katika matumizi ya *YouTube* kwa ujumla, makala haya yanalenga kubainisha aina za maudhui yaliyopo katika video hizo na kutathmini namna yanavyoweza kutumika kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili katika elimu ya vyuo vikuu. Kwa kufanya hivyo, utafiti huu unapanua maarifa kuhusu matumizi ya maudhui ya kidijitali katika ufundishaji wa Kiswahili na kutoa msingi wa uteuzi wa maudhui yanayokidhi malengo ya kozi.

Mapitio ya maandishi yanaonyesha kuwa tafiti nyingi zimechunguza matumizi ya *YouTube* kama jukwaa la kufundishia na kujifunzia katika taaluma mbalimbali, hususan katika ufundishaji wa lugha za kigeni kama Kiingereza. Tafiti hizo zimeonyesha kuwa matumizi ya video huongeza ushiriki wa wanafunzi, motisha ya kujifunza na ujifunzaji wa kujitegemea (Alawiyah na Santosa, 2022; Jailani, 2022). Hata hivyo, tafiti hizo zimejikita zaidi katika matumizi ya *YouTube* kama teknolojia ya ufundishaji kuliko kuchanganua yaliyomo katika video zinazotumiwa kufundishia lugha.

Aidha, maandishi yaliyopo hayatoi maelezo ya kutosha kuhusu aina za maudhui ya Kiswahili yanayopatikana katika *YouTube*, ubora wake, wala namna yanavyoweza kuendana na malengo ya ufundishaji katika elimu ya vyuo vikuu. Pengo hili linaonekana zaidi katika muktadha wa vyuo vikuu nchini Kenya, ambako ushahidi wa kisayansi kuhusu maudhui ya *YouTube* kwa ajili ya kufundishia Kiswahili bado ni mdogo.

Kwa msingi huo, makala haya yanajaza pengo hilo kwa kuchanganua yaliyomo katika video 44 za *YouTube* pamoja na maoni ya wanafunzi 87 na wahadhiri 10 wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Utafiti huu unapanua maarifa kuhusu aina za maudhui yanayopatikana katika *YouTube*, namna yanavyoweza kutumika katika ufundishaji wa Kiswahili, na mambo ambayo wahadhiri wanapaswa kuzingatia wanapochagua maudhui ya kidijitali kwa ajili ya kufanikisha ujifunzaji.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulitumia mkabala mseto uliounganisha data za kiasi na data za ubora ili kutoa uelewa mpana kuhusu yaliyomo katika jukwaa la *YouTube* kama wenzo wa kufundishia Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya. Mkabala huu uliteuliwa kwa sababu uliwezesha kukusanya ushahidi kutoka kwa vyanzo mbalimbali, yaani wanafunzi, wahadhiri na video za *YouTube*, hivyo kuongeza uhalali na ukamilifu wa matokeo ya utafiti (Creswell & Creswell, 2018).

Kwa upande wa data za kiasi, hojaji zilitumika kukusanya taarifa kutoka kwa wanafunzi kuhusu matumizi yao ya maudhui ya *YouTube* katika ujifunzaji wa Kiswahili. Vilevile, hojaji zilitumiwa kwa wahadhiri ili kupata taarifa kuhusu matumizi yao ya *YouTube* katika ufundishaji wa Kiswahili, huku uchanganuzi wa yaliyomo katika video za *YouTube* ukitumika kubainisha aina za maudhui yaliyokuwapo na namna yalivyoweza kutumika katika ufundishaji wa Kiswahili. Muunganiko wa mbinu hizi uliwezesha kulinganisha mitazamo ya washiriki na ushahidi uliopatikana moja kwa moja kutoka katika maudhui ya video.

Aidha, uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika kama mbinu kuu ya kuchambua video 44 zilizochaguliwa kutoka *YouTube*. Mbinu hii ilifaa kwa sababu iliruhusu kutambua, kuainisha na kufasiri maudhui yaliyowasilishwa katika video kwa kuzingatia vipengele vya ufundishaji wa Kiswahili. Kwa mujibu wa Braun na Clarke (2022), uchanganuzi wa kimaudhui na wa yaliyomo hutoa utaratibu wa kubainisha ruwaza na mada zinazojitokeza katika data za ubora, hivyo kufaa katika tafiti zinazolenga kuelewa maudhui ya kidijitali.

Kwa kutumia mkabala huu, utafiti uliweza kuunganisha ushahidi wa kitakwimu na wa kimaelezo ili kujibu lengo la utafiti kuhusu yaliyomo katika jukwaa la *YouTube* kama wenzo wa kufundishia Kiswahili. Utafiti huu ulifanyika katika Chuo Kikuu cha Kibabii, kilichopo Kaunti ya Bungoma nchini Kenya. Chuo hiki kilichaguliwa kimakusudi kwa kuwa ni mojawapo ya taasisi za elimu ya juu zinazotoa programu za Kiswahili na zinazohimiza matumizi ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, wahadhiri na wanafunzi wa Kiswahili katika chuo hiki hutumia majukwaa mbalimbali ya kidijitali, ikiwemo *YouTube*, kama nyenzo ya kufundishia na kujifunza, jambo lililokifanya kuwa mazingira mwafaka ya kuchunguza yaliyomo katika

jukwaa hilo na mchango wake katika ufundishaji wa Kiswahili.

**Jedwali 1: Vyanzo vya Data na Madhumuni yake**

| **Kundi la Washiriki/Vyanzo vya Data** | **Idadi** | **Mbinuya Ukusanyaji Data** | **Madhumuni** |
|---|---|---|---|
| Wanafunzi wa Kiswahili | 87 | Hojaji | Kubainisha matumizi na mitazamo kuhusu maudhui ya *YouTube* |
| Wahadhiri wa Kiswahili | 10 | Hojaji | Kubainisha uzoefu wa kutumia *YouTube* katika ufundishaji |
| Video za *YouTube* | 44 | Uchanganuzi wa yaliyomo | Kubainisha aina za maudhui ya Kiswahili yaliyopo |

Jedwali 1 linaonyesha kuwa data za utafiti zilitokana na vyanzo vitatu. Hojaji zilitumika kukusanya taarifa kutoka kwa wanafunzi 87 na wahadhiri 10 kuhusu matumizi ya *YouTube* katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Aidha, video 44 za *YouTube* zilichanganuliwa ili kubainisha aina za maudhui yaliyomo na namna yanavyoweza kutumika kama wenzo wa kufundishia. Muunganiko wa taarifa kutoka kwa washiriki na uchanganuzi wa video uliwezesha kulinganisha mitazamo ya watumiaji na maudhui halisi yaliyopatikana katika jukwaa la *YouTube*.

Kwa upande wa data za ubora, hojaji zilijumuisha maswali ya wazi yaliyowapa washiriki nafasi ya kueleza mitazamo yao kuhusu matumizi ya *YouTube* katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Aidha, uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika kuchunguza video 44 za *YouTube* ili kubainisha aina za maudhui yaliyowasilishwa. Muunganiko wa data hizi uliwezesha kulinganisha mitazamo ya washiriki na ushahidi uliotokana na maudhui ya video.

Utafiti huu ulitumia mbinu ya usampulishaji wa kimakusudi katika uteuzi wa washiriki na video za *YouTube*. Mbinu hii iliteuliwa kwa kuwa ilimwezesha mtafiti kuchagua vyanzo vya data vilivyokuwa na uwezo wa kutoa taarifa zinazohusiana moja kwa moja na madhumuni ya utafiti (Creswell, 2018; Patton, 2015). Wanafunzi na wahadhiri walichaguliwa kwa sababu walijihusisha moja kwa moja na ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kibabii. Aidha, video 44 za *YouTube* ziliteuliwa kimakusudi kwa kuwa zilihusu maudhui ya ufundishaji wa Kiswahili na zilitosheleza vigezo vya utafiti kuhusu yaliyomo katika jukwaa hilo. Uteuzi huu ulihakikisha kuwa data iliyokusanywa ilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na lengo la utafiti, ambalo lililenga kuchunguza aina za maudhui yanayopatikana katika *YouTube* kama wenzo wa kufundishia Kiswahili.

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia hojaji na fomu ya uchanganuzi wa yaliyomo. Hojaji zilitumika kukusanya taarifa kutoka kwa wahadhiri na wanafunzi wa Kiswahili juu ya matumizi ya *YouTube* kama wenzo wa kufundishia na kujifunza Kiswahili. Hojaji zilijumuisha maswali funge yaliyowezesha ukusanyaji wa data za kiasi pamoja na maswali wazi yaliyowapa washiriki nafasi ya kueleza maoni yao kuhusu maudhui ya *YouTube*.

Aidha, fomu ya uchanganuzi wa yaliyomo ilitumika kuchunguza video 44 za *YouTube* zilizochaguliwa kimakusudi. Fomu hiyo iliundwa kwa kuzingatia lengo la utafiti na ilijumuisha vipengele vya maudhui vilivyohusiana na ufundishaji wa Kiswahili, kama vile sarufi, fasihi, matamshi, mawasiliano ya lugha na maudhui mengine ya kielimu. Matumizi ya zana hizi mbili yaliwezesha kulinganisha taarifa za washiriki na ushahidi uliopatikana kutoka katika video zilizochanganuliwa.

Ili kuhakikisha ubora wa data zilizokusanywa, hojaji na fomu ya uchanganuzi wa yaliyomo ziliandaliwa kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti na kupitia mapitio ya

maandishi husika. Vilevile, zana hizo zilifanyiwa uhakiki na wataalamu wa lugha na mbinu za utafiti ili kuthibitisha kuwa zilikuwa zinapima vipengele vilivyokusudiwa. Aidha, matumizi ya vyanzo tofauti vya data, zikiwemo hojaji kutoka kwa wanafunzi na wahadhiri pamoja na uchanganuzi wa video za *YouTube*, yalisaidia kuongeza uaminifu na uthabiti wa matokeo kupitia uthibitishaji mtambuko (triangulation).

Data za kiasi zilizopatikana kupitia hojaji zilichanganuliwa kwa kutumia takwimu za kimaelezo, hususan masafa na asilimia, ili kuonyesha mwelekeo wa majibu ya washiriki. Matokeo yaliwasilishwa kwa kutumia majedwali kwa lengo la kurahisisha uelewa wa taarifa. Kwa upande wa data za ubora, majibu ya maswali wazi na maudhui ya video 44 za *YouTube* yalichanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi wa yaliyomo. Katika uchanganuzi huu, maudhui yaliainishwa katika kategoria zilizoibuka kutokana na lengo la utafiti, zikiwemo sarufi, fasihi, matamshi, mawasiliano ya lugha na maudhui mengine ya kielimu. Kategoria hizo zilitumika kueleza namna *YouTube* inavyoweza kutumika kama wenzo wa kufundishia Kiswahili katika elimu ya vyuo vikuu.

## MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inawasilisha matokeo yaliyopatikana kutokana na uchambuzi wa data za hojaji kutoka kwa wanafunzi 87 na wahadhiri 10 pamoja na uchanganuzi wa video 44 za *YouTube*. Matokeo yanawasilishwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na kujadiliwa kwa kuhusishwa na maandishi yaliyotangulia pamoja na Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi.

**Jedwali 2: Usambazaji wa Maudhui katika Video za *YouTube* Zilizochanganuliwa**

| Maudhui | Idadi ya Video | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Sarufi | 16 | 36.4 |
| Fasihi (Simulizi na Andishi) | 10 | 22.7 |
| Matamshi na Mawasiliano | 8 | 18.2 |
| Hotuba, Ushairi na Maigizo | 10 | 22.7 |
| **Jumla** | **44** | **100.0** |

Jedwali 2 linaonyesha kuwa video 44 zilizochanganuliwa zilikuwa na maudhui mbalimbali yanayohusiana na ufundishaji wa Kiswahili. Maudhui ya sarufi yalionekana kwa wingi zaidi, yakijumuisha video 16 (asilimia 36.4), yakifuatiwa na fasihi simulizi na andishi ambazo zilikuwa video 10 (asilimia 22.7). Aidha, video zilizohusu matamshi na mawasiliano ya lugha zilikuwa 8 (asilimia 18.2), ilhali video za hotuba, ushairi na maigizo zilikuwa 10 (asilimia 22.7).

Kwa ujumla, matokeo haya yanaonyesha kuwa *YouTube* ina hazina pana ya maudhui yanayoweza kutumiwa katika kufundishia vipengele mbalimbali vya Kiswahili, ingawa mgawanyo wake unatofautiana kulingana na aina ya maudhui. Matokeo haya yanaonyesha kuwa watayarishaji wa maudhui ya Kiswahili katika YouTube wameelekeza juhudi kubwa katika utayarishaji wa video zinazohusu sarufi. Hali hii inaweza kuelezwa na umuhimu wa sarufi kama msingi wa umahiri wa lugha na changamoto ambazo wanafunzi hukutana nazo katika kuelewa kanuni za kisarufi. Uwepo wa video nyingi za sarufi unaonyesha kuwa *YouTube* imekuwa jukwaa muhimu la kutoa maelezo ya ziada yanayokamilisha ufundishaji wa darasani.

Aidha, uwepo wa video za fasihi, matamshi, mawasiliano, ushairi, maigizo na hotuba unaonyesha kuwa maudhui yaliyomo katika *YouTube* hayaishii kwenye kufundisha kanuni za lugha pekee, bali pia yanahusisha matumizi halisi ya Kiswahili katika miktadha ya kitaaluma, kijamii na kiutamaduni. Hivyo, wanafunzi hupata nafasi ya kuona matumizi ya lugha katika mazingira halisi, jambo linalochangia kukuza uelewa na umahiri wa lugha.

Matokeo haya yanaafikiana na Mayer (2021) ambaye anaeleza kuwa ujifunzaji kwa kutumia multimedia huongeza uelewa kwa kuunganisha picha, sauti na maandishi. Vilevile, Berk (2009) anasisitiza kuwa video za kielimu huongeza ushiriki wa wanafunzi na hurahisisha uelewa wa dhana changamani. Kwa mtazamo wa Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi, utofauti wa maudhui yaliyopo katika *YouTube* unaongeza manufaa yanayoonekana kwa watumiaji, hivyo kuhamasisha wahadhiri na wanafunzi kuyakubali na kuyatumia katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Kwa hiyo, matokeo haya yanathibitisha kuwa *YouTube* ni zaidi ya jukwaa la kuhifadhi video; ni hazina ya maudhui ya

kielimu inayoweza kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili iwapo maudhui yake yatachaguliwa kwa kuzingatia ubora, usahihi na ulinganifu wake na malengo ya mtaala.

**Jedwali 3: Maudhui ya Sarufi Yaliyobainika katika Video za *YouTube***

| **Kipengele cha Sarufi** | **Idadi ya Video** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| Aina za maneno | 5 | 31.3 |
| Ngeli za nomino | 4 | 25.0 |
| Nyakati | 3 | 18.7 |
| Muundo wa sentensi | 2 | 12.5 |
| Uundaji wa maneno | 2 | 12.5 |
| **Jumla** | **16** | **100.0** |

Jedwali 3 linaonyesha kuwa kati ya video 16 zilizohusu sarufi, mada ya aina za maneno ndiyo ilijitokeza mara nyingi, ikiwa na video 5 (asilimia 31.3). Hii ilifuatiwa na ngeli za nomino, ambazo zilikuwa video 4 (asilimia 25.0). Aidha, mada za nyakati zilijitokeza katika video 3 (asilimia 18.7), ilhali muundo wa sentensi na uundaji wa maneno vilikuwa na video 2 (asilimia 12.5) kila moja.

Matokeo haya yanaonyesha kuwa watayarishaji wa maudhui ya Kiswahili katika *YouTube* wameelekeza juhudi kubwa katika mada za msingi za sarufi zinazowaletea wanafunzi changamoto katika ujifunzaji. Uwepo wa video nyingi kuhusu aina za maneno na ngeli za nomino unaashiria kuwa maeneo hayo yanahitaji ufafanuzi wa ziada unaosaidia wanafunzi kuelewa kanuni za kisarufi kupitia mifano ya kuona na kusikia.

Matokeo haya yanaafikiana na Mayer (2021) anayeeleza kuwa ujifunzaji unaotumia multimedia huongeza uelewa wa dhana changamani kwa kuunganisha maandishi, sauti na picha. Vivyo hivyo, Berk (2009) anabainisha kuwa matumizi ya video za kielimu huwasaidia wanafunzi kuelewa dhana ambazo mara nyingi huwa ngumu kufafanuliwa kwa maandishi pekee. Kwa muktadha wa Kiswahili, video za sarufi huwapa wanafunzi fursa ya kusitisha, kurudia na kufuatilia maelezo kwa kasi yao wenyewe, jambo linalochochea ujifunzaji wa kujitegemea.

Kwa mtazamo wa Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi, upatikanaji wa maudhui mengi ya sarufi katika *YouTube* huongeza manufaa yanayoonekana kwa wahadhiri na wanafunzi. Hali hii huchangia kukubalika kwa *YouTube* kama wenzo wa kufundishia, kwa kuwa huwapa watumiaji rasilimali zinazorahisisha ufundishaji wa vipengele muhimu vya Kiswahili.

**Jedwali 4: Maudhui ya Fasihi Yaliyobainika katika Video za *YouTube***

| **Kipengele cha Sarufi** | **Idadi ya Video** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| Aina za maneno | 5 | 31.3 |
| Ngeli za nomino | 4 | 25.0 |
| Nyakati | 3 | 18.7 |
| Muundo wa sentensi | 2 | 12.5 |
| Uundaji wa maneno | 2 | 12.5 |
| **Jumla** | **16** | **100.0** |

Jedwali 4 linaonyesha kuwa kati ya video 10 zilizochanganuliwa kuhusu fasihi ya Kiswahili, ushairi ndio uliojitokeza kwa wingi zaidi, ukiwakilishwa na video 3 (asilimia 30.0). Maudhui ya tamthilia, riwaya na fasihi simulizi yalikuwa na video 2 (asilimia 20.0) kila moja, huku uhakiki wa kazi za fasihi ukiwakilishwa na video 1 (asilimia 10.0).

Matokeo haya yanaonyesha kuwa watayarishaji wa maudhui ya Kiswahili katika *YouTube* wamejikita zaidi

katika vipengele vinavyofundishwa mara kwa mara katika kozi za fasihi. Uwepo wa video zinazohusu ushairi, tamthilia na riwaya unaonyesha kuwa jukwaa hili linatoa fursa kwa wanafunzi kuona na kusikia utekelezaji wa kazi za fasihi badala ya kuzisoma kwa maandishi pekee. Hali hii huwasaidia kuelewa vipengele kama vile dhamira, wahusika, mtindo, matumizi ya lugha na mbinu za kisanaa kwa uhalisia zaidi.

Aidha, video za fasihi simulizi zina mchango mkubwa katika kuhifadhi na kuwasilisha urithi wa fasihi ya Kiswahili. Kupitia maonyesho ya hadithi, methali, nahau na nyimbo za jadi, wanafunzi huweza kujifunza matumizi ya lugha katika mazingira halisi ya kijamii na kiutamaduni. Hivyo, *YouTube* huongeza fursa za kujifunza zinazovuka mipaka ya darasa la kawaida.

Matokeo haya yanaafikiana na Berk (2009) anayeeleza kuwa matumizi ya video katika elimu huongeza ushiriki wa wanafunzi na hurahisisha uelewa wa dhana zinazohitaji vielelezo vya kuona. Vilevile, Mayer (2021) anaeleza kuwa ujifunzaji wa multimedia huongeza uwezo wa wanafunzi kuelewa na kukumbuka taarifa kwa kuunganisha sauti, picha na maandishi katika mchakato mmoja wa ujifunzaji.

Kwa mtazamo wa Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi, matumizi ya video za fasihi katika *YouTube* yanaongeza uwiano wa manufaa ikilinganishwa na mbinu za kawaida za ufundishaji, kwa kuwa wanafunzi hupata uzoefu wa moja kwa moja wa kazi za fasihi. Hali hii inaongeza motisha ya kujifunza na kurahisisha upokeaji wa teknolojia hiyo katika ufundishaji wa Kiswahili. Kwa ujumla, matokeo haya yanaonyesha kuwa *YouTube* ni hazina muhimu ya maudhui ya fasihi yanayoweza kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili katika elimu ya vyuo vikuu, mradi wahadhiri wachague video zenye usahihi wa kitaaluma, ubora wa uchambuzi na ulinganifu na malengo ya kozi.

**Jedwali 5: Maudhui ya Matamshi na Mawasiliano Yaliyobainika katika Video za *YouTube***

| **Kipengele** | **Idadi ya Video** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| Matamshi na Lafudhi | 3 | 37.5 |
| Mazungumzo ya Kiswahili | 2 | 25.0 |
| Hotuba na Uwasilishaji | 2 | 25.0 |
| Mahojiano | 1 | 12.5 |
| **Jumla** | **8** | **100.0** |

Jedwali 5 linaonyesha kuwa kati ya video 8 zilizochanganuliwa kuhusu matamshi na mawasiliano ya lugha, matamshi na lafudhi vilijitokeza kwa kiwango kikubwa zaidi, vikijumuisha video 3 (asilimia 37.5). Aidha, mazungumzo ya Kiswahili na hotuba na uwasilishaji vilikuwa na video 2 (asilimia 25.0) kila kimoja, huku mahojiano yakijitokeza katika video 1 (asilimia 12.5).

Matokeo haya yanaonyesha kuwa maudhui ya *YouTube* yanawapa wanafunzi fursa ya kujifunza matumizi halisi ya Kiswahili kupitia mazingira ya mawasiliano yanayowiana na hali za maisha ya kila siku na shughuli za kitaaluma. Kupitia video hizo, wanafunzi husikiliza matamshi sahihi, matumizi ya lafudhi mbalimbali, kiimbo, mkazo pamoja na matumizi ya msamiati katika miktadha tofauti ya mawasiliano. Hali hii huwasaidia kujenga umahiri wa kusikiliza, kuzungumza na kuwasiliana kwa ufasaha.
Aidha, video za mazungumzo na hotuba huwapa wanafunzi nafasi ya kushuhudia matumizi ya Kiswahili katika mazingira halisi badala ya kutegemea maelezo ya kinadharia pekee. Hivyo, *YouTube* huongeza uhalisia wa ujifunzaji kwa kuwaunganisha wanafunzi na matumizi ya lugha katika miktadha ya kijamii, kitaaluma na kiutamaduni.

Matokeo haya yanaafikiana na Jailani (2022) wanaoeleza kuwa matumizi ya *YouTube* huimarisha stadi za kusikiliza na kuzungumza kwa kuwa wanafunzi hujifunza kupitia matumizi halisi ya lugha. Vivyo hivyo, Alawiyah na Santosa (2022) walibaini kuwa wanafunzi wanaotumia *YouTube* huonyesha ongezeko la kujiamini katika matumizi ya lugha pamoja na uboreshaji wa uwezo wa mawasiliano.

Kwa mtazamo wa Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi, maudhui haya yanaongeza uwiano wa manufaa kwa kuwa yanatoa uzoefu wa kujifunza ambao haupatikani kwa urahisi kupitia maandishi pekee. Hivyo, matumizi ya *YouTube* huchangia kukubalika kwa teknolojia hiyo katika ufundishaji wa Kiswahili na kuongeza motisha ya wanafunzi kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji. Kwa ujumla, matokeo haya yanaonyesha kuwa *YouTube* ni wenzo muhimu katika kukuza stadi za matamshi na mawasiliano ya Kiswahili, ingawa wahadhiri wanapaswa kuhakikisha kuwa video wanazoziteua zinazingatia Kiswahili sanifu, usahihi wa kitaaluma na malengo ya kozi.

**Jedwali 6: Maudhui Mengine ya Kielimu Yaliyobainika katika Video za *YouTube***

| **Maudhui** | **Idadi ya Video** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| Mijadala ya Kitaaluma | 3 | 30.0 |
| Semina za Kielimu | 2 | 20.0 |
| Mafunzo ya Uandishi wa Kiswahili | 2 | 20.0 |
| Utamaduni wa Kiswahili | 2 | 20.0 |
| Vipindi vya Elimu | 1 | 10.0 |
| **Jumla** | **10** | **100.0** |

Jedwali 6 linaonyesha kuwa video zilizowekwa katika kundi la maudhui mengine ya kielimu zilikuwa 10. Miongoni mwa maudhui hayo, mijadala ya kitaaluma ndiyo ilijitokeza kwa kiwango kikubwa zaidi, ikiwa na video 3 (asilimia 30.0). Aidha, semina za kielimu, mafunzo ya uandishi wa Kiswahili na maudhui ya utamaduni wa Kiswahili yalikuwa na video 2 (asilimia 20.0) kila moja, huku vipindi vya elimu vikijitokeza katika video 1 (asilimia 10.0).

Matokeo haya yanaonyesha kuwa *YouTube* haiishii kuwa chanzo cha maudhui ya sarufi na fasihi pekee, bali pia hutoa rasilimali zinazowasaidia wanafunzi kujenga ujuzi mpana wa kitaaluma na kiutamaduni. Kupitia mijadala ya kitaaluma na semina mbalimbali, wanafunzi hupata fursa ya kufuatilia hoja za kitaaluma, mbinu za uwasilishaji na matumizi rasmi ya Kiswahili katika mazingira ya elimu ya vyuo vikuu.

Aidha, video zinazohusu utamaduni wa Kiswahili huwasaidia wanafunzi kuelewa uhusiano uliopo kati ya lugha na utamaduni. Ujifunzaji wa Kiswahili hauishii katika kanuni za lugha pekee, bali pia unahusisha kuelewa mila, desturi, maadili na mazingira ya matumizi ya lugha hiyo. Hivyo, *YouTube* hupanua mazingira ya ujifunzaji kwa kuwapa wanafunzi uzoefu unaovuka mipaka ya darasa la kawaida.

Matokeo haya yanaafikiana na Ratna Rintaningrum (2024) anaobainisha kuwa majukwaa ya kidijitali huchochea ujifunzaji shirikishi kwa kuwapa wanafunzi fursa ya kushiriki katika mazingira halisi ya kielimu. Vivyo hivyo, UNESCO inasisitiza kwamba teknolojia za kidijitali huongeza upatikanaji wa rasilimali za kujifunzia na kuimarisha ujifunzaji endelevu katika elimu ya juu.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Msambao wa Uvumbuzi, utofauti wa maudhui yanayopatikana katika *YouTube* huongeza uwezekano wa teknolojia hiyo kukubalika kwa kuwa watumiaji huona manufaa yake katika nyanja mbalimbali za ujifunzaji. Kadiri wahadhiri na wanafunzi wanavyoona matumizi yake katika maeneo tofauti ya Kiswahili, ndivyo uwezekano wa kuendelea kuitumia unavyoongezeka. Kwa ujumla, matokeo haya yanathibitisha kuwa *YouTube* ni hazina pana ya maudhui ya kielimu yanayoweza kutumika kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili katika elimu ya vyuo vikuu, mradi uteuzi wa video uzingatie ubora wa maudhui, usahihi wa taarifa na ulinganifu wake na malengo ya kozi.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Utafiti huu umebaini kuwa *YouTube* ni wenzo muhimu katika ufundishaji wa Kiswahili katika elimu ya juu kutokana na wingi na utofauti wa maudhui yake, hususan katika vipengele vya sarufi, fasihi, matamshi na mawasiliano. Matokeo yanaonyesha kuwa matumizi ya maudhui ya *YouTube* huongeza ushiriki wa wanafunzi, hurahisisha uelewa wa dhana za lugha na huchochea ujifunzaji wa kujitegemea. Hata hivyo, ufanisi wa matumizi yake unategemea ubora wa maudhui, ulinganifu wake na malengo ya mtaala pamoja na uwezo

wa wahadhiri kuyachagua na kuyatumia ipasavyo katika mchakato wa ufundishaji.

**Mapendekezo:** Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu, inapendekezwa kuwa wahadhiri wa Kiswahili wachague na kutumia video za *YouTube* zilizohakikiwa ili kuhakikisha zinaendana na malengo ya kozi na viwango vya kitaaluma. Aidha, vyuo vikuu viendelee kuimarisha miundombinu ya TEHAMA, hususan upatikanaji wa intaneti ya uhakika, na kuwajengea wahadhiri uwezo wa kutumia maudhui ya kidijitali katika ufundishaji. Hatua hizi zitasaidia kuongeza matumizi bora ya *YouTube* na kuboresha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika elimu ya juu, sambamba na mwelekeo mpana wa kubadili mazingira ya ujifunzaji kwa kutumia teknolojia za kidijitali.

**MAREJELEO**


Alawiyah, S., & Santosa, I. (2022). Students' perceptions on the roles of YouTube in improving english speaking skill. *Ijlecr - International Journal OF Language Education and Culture Review*, *8*(2), 99–116. https://doi.org/10.21009/ijlecr.v8i2.32135

Almurashi, W. A. (2016). The effective use of YouTube videos for teaching English language in classrooms as supplementary material at Taibah University in Alula. *International Journal of English Language and Linguistics Research*, *4*(3), 32–47. https://www.researchgate.net/publication/329727456_THE_EFFECTIVE_USE_OF_YOUTUBE_VIDEOS_FOR_TEACHING_ENGLISH_LANGUAGE_IN_CLASSROOMS_AS_SUPPLEMENTARY_MATERIAL_AT_TAIBAH_UNIVERSITY_IN_ALULAAnderson, T. (Ed.). (2008). *The theory and practice of online learning* (2nd ed.). Athabasca University Press.

Berk, R. A. (2009). Multimedia teaching with video clips: TV, movies, YouTube, and mtvU in the college classroom. *International Journal of Technology in Teaching and Learning*, *5*(1), 1–21. https://www.ronberk.com/articles/2009_video.pdf

Bhattacherjee, A. (2012). *Social science research: Principles, methods, and practices* (2nd ed.). University of South Florida.

Braun, V., & Clarke, V. (2022). *Thematic analysis: A practical guide*. SAGE Publications.

Creswell, J. W. (2014). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (4th ed.). SAGE Publications.

Creswell, J. W., & Creswell, J. D. (2018). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (5th ed.). SAGE Publications.

DeWitt, D., Alias, N., Siraj, S., Yaakub, M. Y., Ayob, J., & Ishak, R. (2013). The potential of YouTube for teaching and learning in the performing arts. *Procedia – Social and Behavioral Sciences*, *103*, 1118–1126. https://doi.org/10.1016/j.sbspro.2013.10.439

Flick, U. (2009). *An introduction to qualitative research* (4th ed.). SAGE Publications.

Guo, P. J., Kim, J., & Rubin, R. (2014). How video production affects student engagement: An empirical study of MOOC videos. In *Proceedings of the First ACM Conference on Learning @ Scale Conference* (pp. 41–50). Association for Computing Machinery. https://doi.org/10.1145/2556325.2566239

Jackman, W. M. (2019). YouTube usage in the university classroom: An argument for its pedagogical benefits. *International Journal of Emerging Technologies in Learning*, *14*(9), 157–166. https://doi.org/10.3991/ijet.v14i09.10475

Jaffar, A. A. (2012). YouTube: An emerging tool in anatomy education. *Anatomical Sciences Education*, *5*(3), 158–164. https://doi.org/10.1002/ase.1268

Jailani, A. (2022). The use of YouTube videos in English language teaching: A perspective of indonesian undergraduate students majoring in English language education. *J-Shmic : Journal of English for Academic*, *9*(2), 13–24. https://doi.org/10.25299/jshmic.2022.vol9(2).9949

Kelsen, B. (2009). Teaching EFL to the iGeneration: A survey of using YouTube as supplementary material with college EFL students in Taiwan. *CALL-EJ, 10*(2), 1–18. https://callej.org/index.php/journal/article/view/183/117

Koehler, M. J., & Mishra, P. (2009). What is technological pedagogical content knowledge (TPACK)? *Contemporary Issues in Technology and Teacher Education*, *9*(1), 60–70. https://www.researchgate.net/publication/260281100_What_is_technological_pedagogical_content_TPACK

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques* (2nd ed.). New Age International Publishers.

Mayer, R. E. (2009). *Multimedia learning* (2nd ed.). Cambridge University Press.

Mayer, R. E. (2021). *Multimedia learning* (3rd ed.). Cambridge University Press.

Merriam, S. B., & Tisdell, E. J. (2016). *Qualitative research: A guide to design and implementation* (4th ed.). Jossey-Bass.

Miles, M. B., Huberman, A. M., & Saldaña, J. (2020). *Qualitative data analysis: A methods sourcebook* (4th ed.). SAGE Publications.

Patton, M. Q. (2015). *Qualitative research & evaluation methods* (4th ed.). SAGE Publications.

Ratna Rintaningrum. (2024). Technology enable language learning: Mediating role of Collaborative learning. *Lingeduca Journal of Language and Education Studies*, *3*(1), 1–20. https://doi.org/10.55849/lingeduca.v3i1.706

UNESCO. (2020). *Education in a post-COVID world: Nine ideas for public action*. UNESCO. https://unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000373717

Zhang, D., Zhou, L., Briggs, R. O., & Nunamaker, J. F. (2006). Instructional video in e-learning: Assessing the impact of interactive video on learning effectiveness. *Information & Management, 43*(1), 15–27. https://doi.org/10.1016/j.im.2005.01.004